East African Journal of Swahili Studies, Volume 6, Issue 1, 2023
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1556

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 6, Issue 1, 2023
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Taswira ya Distopia katika Riwaya ya Kimajaribio ya Kiswahili: Mfano wa Riwaya ya Bina-Adamu na Dunia Yao

*Mwove Phyllis Mwende[1*] na Alex Umbima Kevogo[2]*

[1] Chuo Kikuu cha Mount Kenya, S. L. P. 342-01000 Thika, Kenya
[2] Chuo Kikuu cha Garissa, S. L. P. 1801 – 70100 Garissa, Kenya
[*] Barua pepe ya mawasiliano: mutuaphyllis1@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1556**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*05 Novemba 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Distopia, Riwaya ya Kimajaribio, Taswira, Utandawazi.*

**IKISIRI**

Mustakabali wa Bara la Afrika umekuwa suala la msingi katika maudhui ya riwaya ya kisasa ya Kiswahili. Fasihi ya kimajaribio inayoakisi hali za kidistopia inachora taswira hasi za mustakabali wa Bara la Afrika. Mazingira ya kidistopia ni mandhari yanayokabiliwa na kila aina ya matatizo au uovu uliokithiri ambayo huwa ya kiubunifu. Dhana hii hutumiwa kueleza jamii ambayo sheria zake hubadilishwa na kuishia kuwa za kuwadhalilisha wanajamii kupita kiasi. Kwa ujumla, wanajamii wanaojipata kwenye ulimwengu wa aina hii huwa kwenye njiapanda. Wanajamii hao huwa wamekwisha poteza tumaini la kuishi kutokana na dhuluma zinazowakabili. Baadhi yao hutamaushwa na ugumu wa maisha na kutamani kuangamia au kujiangamiza ili kuepuka ulimwengu huo wa shida. Kazi za fasihi zinazofuata mkondo wa kidistopia hudhamiria kutoa tahadhari au kuhamasisha jamii kuwajibika ili kuepuka maangamizi yanayokuja. Kazi hizo ni za utabiri wa mambo yanayoweza kutokea baadaye. Makala hii inakusudia kuonyesha jinsi taswira ya kidistopia inavyojitokeza katika riwaya ya kimajaribio ya Kiswahili kwa kutumia Nadharia ya Usasabaadaye ilioasisiwa na Linda Hutcheon na kufafanuliwa zaidi na Patricia Waugh. Riwaya mbili za kimajaribio; Dunia Yao (2006) ya Said Ahmed Mohamed na Bina-Adamu! (2002) ya Kyallo Wadi Wamitila zilitueliwa kimaksudi ili kuonyesha jinsi taswira ya distopia inavyobainika. Utafiti ulifanywa maktabani. Data ilikusanywa kutokana na usomaji wa kina wa riwaya teule ulioongozwa na mihimili ya Nadharia ya Usasabaadaye. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya kimaelezo kwa mujibu wa Nadharia ya Usasabaadaye. Matokeo ya utafiti yanabainisha kuwa waandishi wana sababu za kimsingi za kusawiri mandhari ya kidistopia ili kutoa taswira kamili ya nchi za Kiafrika katika muktadha wa baada ya ukoloni chini ya utandawazi, mfumo wa soko huria, ubeberu mpya, ubinafsi, taathira za kigeni na uporomokaji wa kasi wa nguzo za maisha ya Kiafrika.

**APA CITATION**

Mwende, M. P. & Kevogo, A. U. (2023). Taswira ya Distopia katika Riwaya ya Kimajaribio ya Kiswahili: Mfano wa Riwaya ya Bina-Adamu na Dunia Yao. *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 435-447. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1556.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1556

**CHICAGO CITATION**

Mwende, Mwove Phyllis and Alex Umbima Kevogo. 2023. "Taswira ya Distopia katika Riwaya ya Kimajaribio ya Kiswahili: Mfano wa Riwaya ya Bina-Adamu na Dunia Yao". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 435-447. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1556.

**HARVARD CITATION**

Mwende, M. P. & Kevogo, A. U. (2023) "Taswira ya Distopia katika Riwaya ya Kimajaribio ya Kiswahili: Mfano wa Riwaya ya Bina-Adamu na Dunia Yao", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 435-447. doi: 10.37284/jammk.6.1.1556.

**IEEE CITATION**

M. P. Mwende & A. U. Kevogo "Taswira ya Distopia katika Riwaya ya Kimajaribio ya Kiswahili: Mfano wa Riwaya ya Bina-Adamu na Dunia Yao", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 435-447, Nov. 2023.

**MLA CITATION**

Mwende, Mwove Phyllis & Alex Umbima Kevogo. "Taswira ya Distopia katika Riwaya ya Kimajaribio ya Kiswahili: Mfano wa Riwaya ya Bina-Adamu na Dunia Yao". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Nov. 2023, pp. 435-447, doi:10.37284/jammk.6.1.1556.

## UTANGULIZI

Uandishi wa riwaya za kimajaribio una historia ndefu. Kwa mujibu wa mawazo ya Barth (1984), chimbuko lake linahusishwa na mataifa ya Kimagharibi; Bara Uropa na Marekani. Baadaye katika karne ya ishirini, waandishi Waafrika walianza kuhusika katika uandishi wa fasihi ya kimajaribio. Kazi nyingi za fasihi zilizoandikwa zilishughulikia matatizo yaliyotawala katika dunia nzima baada ya vita vya pili vya dunia pamoja na mustakabali wa jamii kimaisha. Baudrillard (1988) anarai kuwa riwaya ya kisasa iliyoakisi majaribio ilimulika jamii jinsi ilivyo na kusawiri jamii ya kisasa kwa misingi ya kifantasia. Rettova (2016) anaelezea kuwa katika uandishi wa riwaya za kimajaribio watunzi wamefanya majaribio ya kubadilisha, kuvunja, na kukiuka kimaksudi kaida za jadi za uandishi hasa zile zinazohusiana na uhalisia. Bertoncini (2016) anaongezea kuwa riwaya hizo huwa changamano kimuundo.

Kwa mujibu wa Ignatowicz (2007), baadhi ya kazi za fasihi zinazozingatiwa kuwa za kimajaribio ambazo zilitungwa katika jamii za Kimagharibi ni pamoja na: *The Brave New World* (1932) ya Aldous Huxley, *The Animal Farm* (1945) ya George Orwell na *The Handmaids Tale* (1985) ya Margaret Atwood. Kwa upande mwingine, Kevogo (2016) anaeleza kuwa, baadhi ya kazi za kifasihi zinazozingatiwa kuwa za kimajaribio ambazo ziliandikwa na Waafrika ni: *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) za Euphrase Kezilahabi, *Walenisi* (1995) ya Katama Mkangi, *Babu Alipofufuka* (2001) na *Dunia Yao* (2006) za Said Ahmed Mohamed, *Bina-Adamu!* (2002), *Musaleo* (2004) na *Unaitwa Nani?* (2008) za K. W. Wamitila, *Mafamba* (2008) na *Watu wa Gehena* (2012) za Tom Olali.

Waandishi wa fasihi ya kimajaribio inayoakisi mandhari ya kidistopia hulenga matukio yanayowatia hofu wanajamii na kushambulia maadui sugu wanaotishia kuangamiza ulimwengu wa kisasa kwa mfano utandawazi na athari za mifumo ya maisha na tamaduni za kigeni. Pia huangazia masuala nyeti kuhusu jamii na mataifa ya ulimwengu kwa kutumia mbinu ya mafumbo kusimba ujumbe wao pamoja na kuyanasua maisha ya binadamu kutoka kwenye maangamizi. Gromov (2014) anaelezea kuwa waandishi wa fasihi ya Kiswahili inayoakisi hali za kidistopia, katika kazi zao, wanatabiri maafa makubwa ya siku za usoni, dunia kabla na baada ya kuangamia kwa ulimwengu unaongozwa na mamlaka ya kiimila, baa la njaa na umasikini uliokithiri.

*Bina-Adamu!* na *Dunia Yao* ni miongoni mwa riwaya za kimajaribio zinazotumia taswira kama mbinu kuu ya uandishi kutoa ujumbe kwa msomaji. Wamitila (2002), anaeleza taswira kuwa ni maneno yanayojenga hali au picha fulani akilini mwa hadhira. Anaendelea kusema kuwa kuna taswira kuu, taswira mwendo, taswira mguso, taswira mnuso, taswira za kiishara na taswira za usikivu. Waandishi hutumia mbinu hii kumchochea msomaji kuona hali fulani bayana na kumwezesha kuzielewa hisia fulani au kuusimba

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1556

ujumbe unaoweza kusababisha madhara iwapo utatolewa hadharani.

Waandishi wa riwaya ya Kiswahili ya kimajaribio hutumia taswira ya distopia kuonyesha jinsi mataifa mbalimbali barani Afrika yalivyodidimia katika nyanja nyingi ukiwemo uchumi ambao umetokana na mfumo mbaya uliotawaliwa na utegemezi wa misaada, matumizi mabaya ya sayansi na teknolojia pamoja na uongozi mbaya uliozuka baada ya wakoloni kuondoka barani (Diegner, 2016).

Waandishi wa fasihi ya kimajaribio hutumia wahusika jumui na wahusika picha ili kusawiri hali za kidistopia na maudhui ya baada ukoloni katika kazi zao. Kulingana na Wanausasabaadaye, wahusika wanaotumika kwenye riwaya za kisasa za kimajaribio huwa hawaishi katika ulimwengu unaolingana moja kwa moja na ulimwengu halisi tunaouelewa. Waandishi huwasilisha kazi zao kwa njia ya kifantasia kimaksudi ili kuyaangazia upya mambo ya kijamii yanayofanyika kwa njia ya uhalisiajabu (Kevogo, 2016). Mbinu ya uhalisiajabu ni mojawapo wa mbinu za kisanaa zilizotumika kusawiri hali za kidistopia ambapo masimulizi ya kutatanisha yanatekelezwa na wahusika wa kimazingaombwe huku wakisababisha uwasilishaji wa ujumbe kwa njia isiyodhahiri kwa wasomaji.

Waandishi hutumia lugha yenye mvutogubi iliyosheheni matumizi ya mafumbo na istiari. Lugha yao wanayotumia waaandishi ina mnasaba na utandawazi; isitoshe, inaakisi mabadiliko ya kasi yanayodhihirika katika karne hii ya ishirini na moja (Kevogo, 2016). Uandishi wa aina hii hukiuka sheria za uandishi zilizotumika katika fasihi ya kimapokeo. Lengo kuu la makala ni kuonyesha taswira za distopia zinavyosawiriwa katika riwaya za *Bina-Adamu* na *Dunia Yao* kupitia ili kuonyesha maudhui ya kibaadaukoloni yanayojitokeza katika kazi hizo.

**Misingi ya Nadharia ya Usasabaadaye**

Utafiti huu utatumia Nadharia ya Usasabaadaye iliyoasisiwa na Linda Hutcheon (1988) na kufafanuliwa zaidi na Patricia Waugh (2002). Nadharia hii ilitumika katika ukusanyaji, uchanganuzi, ufasiri na uelezaji wa kina wa data na matokeo muhimu ya utafiti kwa mujibu wa malengo ya utafiti. Mihimili yote ya Nadharia ya Usasabaadaye ilitumika katika utafiti huu. Kwa mujibu wa Hutcheon (1988) na Waugh (2002), Nadharia ya Usasabaadaye hutumiwa kuhakiki fasihi ya kimajaribio na huongozwa na mihimili ifuatayo:

- Dhamira: Kazi za fasihi zilizoandikwa kwa kuzingatia mwelekeo huu hushughulikia matatizo yanayoukabili ulimwengu wetu wa kisasa kwa mfano: taathira za utandawazi, biashara ya kimataifa, mmomonyoko wa maadili na athari za kigeni, uchafuzi wa mazingira na athari za ubepari na ubeberu mpya.
- Matumizi ya lugha: Baadhi ya sifa za matumizi ya lugha katika kazi za fasihi zinazozingatia mwelekeo wa usasabaadaye katika uandishi wake ni kama vile:
    - Utouzoefu/Uajinabishaji**:** Huu ni mchezo wa lugha unaohusu kuchangamsha lugha na kuitia lugha uvuguvugu ili ionekane mpya au ngeni kuliko ilivyokuwa, lengo kuu likiwa kubadilisha mtazamo wa msomaj kwa kumwonesha ujumi wa lugha ambao utachukuwa makini ya msomaji; kumvuta kisanaa na kumfanya afikiri zaidi.
    - Mvutogubi: mvutogubi ni mjazo wa jazanda/taswira zenye fumbo, nguvu na mapigo ya kishairi ambayo mara kadhaa huonekana ni muhimu zaidi kuliko maana ingawa kwenye kazi ya fasihi maana bado inabaki kuimarishwa.
    - Lugha ya utandawazi**:** Lugha ya aina hii inatokana na kutokuwa na uhakika kuhusu elimu, matibabu, chakula, makazi, heshima ya mtu, nchi, uraia wake na Uafrika kwa jumla. Ni lugha inayosheheni athari za utandawazi na uwezo wake wa kuharibu utambulisho wa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1556

watu katika viwango mbalimbali kwa mfano kibinafsi, kitaifa na kisiasa.

- Matumizi ya mbinu za lugha zenye mnasaba na utandawazi. Mifano ya matumizi ya lugha yenye mnasaba na utandawazi ni kama vile:
    - Kubuni maneno mapya
    - Kukopa maneno ya kigeni
    - Uvunjaji wa kanuni
    - Matumizi ya sanaa hati

- Wahusika**:** matumizi ya wahusika-picha wanaoibuka ghafla na kuwa viumbe wenye uhai na urani jinsi walivyo binadamu wa kawaida. Waandishi hutumia pia wahusika halisi ambao hupitia tajriba ya binadamu wa kawaida.
- Usimulizi: riwaya nyingi za usasabaadaye hutumia polifoni yaani sauti nyingi zinazosimulia kwa wakati mmoja. Kwa mfano matumizi ya nafsi ya kwanza na msimulizi maizi anayesimulia aliyoyashuhudia au aliyasimuliwa.
- Msuko/ploti: msuko wa riwaya ya usasabaadaye huathiriwa na matumizi ya mbinu zifuatazo:
    - Matumizi ya motifu**:** motifu dhana inayorudiwarudiwa katika kazi ya fasihi ili kusisitiza dhamira ya mtunzi wa kazi ya fasihi. Waandishi wengi wa usasabaadaye hutumia motifu ya safari. Katika riwaya ya *Bina-Adamu* mwandishi ametumia motifu ya safari ambapo mhusika mkuu binadamu anasafiria kwa njia mbili ile ya wakati na ya maeneo.
    - Muaradha**:** istilahi hii inatumiwa kuelezea kazi ya fasihi ambayo ni tokeo la kuletwa pamoja kwa sehemu, maneno, sentensi na vifungu vya waandishi mbalimbali. Muaradha huweza kutokea pale ambapo kazi fulani kwa mfano riwaya inaandikwa kwa kiasi kikubwa katika sifa za mwandishi fulani.
    - Wigobezi: dhana inayotumiwa kuelezea kazi ambayo imeandikwa katika misingi dhahiri ya kuiga kazi nyingine kwa lengo la kuibeza kazi asilia.
    - Mwingilianomatini**:** mwingilianomatini ni ile hali ambapo kazi moja ya fasihi inahusiana na kazi nyingine kwa mfano dhamira, usawiri wa wahusika, matumizi ya lugha na mbinu za sanaa.
    - Mchanganyo ndimi**:** mchanganyondimi ni ile hali ya riwaya ya usasabaadaye kusomba na kujaza kila aina ya taaluma kwenye matini yake. Kwa mfano historia, falsafa, uchumi, siasa, utamaduni, muziki, visasili na dini. Kazi za usasabaadaye pia hupokea athari za fasihi simulizi.
    - Uhalisiamazingaombwe/Uhalisiajabu: uhalisiamazingaombwe ni aina ya fantasia lakini ni mbinu inayoleta dunia mbili pamoja za ukale na usasa. Ukale wenye misingi ya mazingaombwe au ukweli ambao hauwezi kuelezwa kwa mantiki ya nchi za ulaya na usasa unaojaa taathira za kitamaduni, kisayansi na teknolojia inayoletwa wakati wa ukoloni na wakati wa baada ya ukoloni.
    - Ufabulishaji: ufabulishaji ni matumizi ya mbinu za kiistiari na athari za uhalisiafifi zinazohusishwa na kazi za fasihi zinazoainishwa.

Utafiti huu uliweza kuongozwa na malengo mahususi matatu yaliyoweza kushughulikiwa kwa mujibu wa nadharia ya usasabaadaye. Mihimili ya Nadharia hii ilimwongoza mtafiti katika kukusanya data, kuichanganua data na kuifafanua data yenyewe. Mtafiti aliweza kubainisha taswira za kidistopia kwa kuongozwa na mihimili ya matumizi ya lugha na usawiri wa wahusika. Pili, aliweza kujadili na kuwasilisha mbinu za kisanaa zilizoweza kutumiwa na waandishi wa riwaya

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1556

teule kupitia kwa dhamira ya mwandishi na baadaye akaweza kijadili uhusiano wa hali za kidistopia na maudhui kwa njia ya usimulizi na wahusika

### Taswira ya Distopia na Maudhui ya Baadaukoloni katika Riwaya ya *Dunia Yao* na *Bina-Adamu*

Taswira ya distopia inaweza kuelezewa kuwa ni picha inayojitokeza mawazoni mwa msomaji kutokana na matumizi ya tamathali za usemi, istiari na ishara zinazohusiana na mawazo, dhana, vitu au maumbile yanayosimuliwa na mwandishi wa kazi ya fasihi. Kazi hiyo ya fasihi ni ile inayotawaliwa na matatizo ya kila aina pasipo kuwa na matumaini katika maisha ya ulimwengu wa kidhahania (Diegner, 2016).

Wamitila (2002) anaelezea maudhui kuwa ni jumla ya maswala yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi na hujengwa kwenye misingi ya dhamira. Kipindi cha baadaukoloni kinarejelea wakati ambapo wakoloni walikwisha kuondoka barani Afrika na Waafrika kupata uhuru. Taathira ya ukoloni inayoendelea kushuhudiwa barani Afrika ni ile ya ukoloni mamboleo. Hili linaashiria kuwa, baada ya wakoloni kuondoka; kuna athari za ukoloni zilizondelezwa na viongozi Waafrika walioendeleza dhuluma dhidi ya Waafrika wenzao (Kevogo, 2016). Mifumo ya ukoloni ilihakikisha kuwa baadhi ya mataifa ya Afrika yaliendelea kutegemea mataifa ya magharibi ili kujiendeleza.

Kimaudhui, waandishi wa riwaya za *Dunia Yao* na *Bina-Adamu* wamevuka mipaka ya kitaifa ili kudadisi masula anuwai ya kiulimwengu yanayoweka wazi hali ya distopia inayoshuhudiwa katika jamii ya Kiafrika baada ya ukoloni. Maudhui yanayofungamana na taswira za kidistopia ni haya yafuatayo:

### Umaskini Uliokithiri

Kupitia kwa ubunifu wa hali ya juu, waandishi wa riwaya ya kidistopia wamesawiri mataifa yanayoendelea kwa misingi ya uhitaji au ulitima uliokithiri. Bara la Afrika linaonyeshwa kama lililoghubikwa katika umasikini uliokithiri. Hali ya uhitaji inazua hofu na hata kuchangia kusambaratika kwa misingi ya umoja na utangamano wa kifamilia kama vile familia ya Ndi- na familia ya Ndera. Mwandishi anaeleza kuwa:

> *…kisima chake cha pesa kimekauka…kubwa zaidi mkewe Masika au kwa jina maarufu Kisura, kamkimbia. Kachupia farasi mwenye soji jema kwenda ng'ambo nyingine ya uchumi* (Mohamed, 2006, uk. 120)

Kutokana na dondoo hili ni wazi kuwa baada ya Ndera kuishiwa na mali, mkewe anamtoroka na kumwacha kwenye njiapanda; anakwenda kutafuta malezi na mapenzi kwengine. Mohamed (2006) ametumia baadhi ya familia kuonyesha jinsi umaskini unaweza kusabaratisha familia na kusababisha utengano huku wnafamilia wakitoroka kwao na kuhamia kwengine. Wengine wanaamua kuishi maisha ya ubinafsi kwa maana hawataki kuwa tegemeo la ndugu zao. Taswira ya utovu wa maadili unaosababishwa na umasikini inaakisiwa katika dondoo lifuatalo:

> *Akiondoka huyu maisha yatatunyookea. Hatimaye akaondoka. Wenyewe tulibakia Kuibaiba kalamu katika ofisi zetu. Wasafiri…kukwepa kulipa nauli. Wakuu wa shule kuyachukua madaftari ya shule kuwapelekea watoto wao. Wakusanya sadaka walidokoa na kuzifutika noti mifukoni* (Wamitila, 2002, uk. 154)

Mwandishi anaeleza matatizo yanayotokana na kutoweza kutimiza mahitaji muhimu; hali ambayo inazidi kudidimiza baadhi ya sekta muhimu kama vile elimu, usafiri na dini katika kijiji cha Zakongwe inayosimamia bara la Afrika. Matendo kama haya yanadhoofisha maendeleo, maadili na kukuza umaskini zaidi nchini.

### Uchafuzi wa Mazingira

Riwaya ya kidostopia inasawiri uchafuzi wa mazingira kupitia kwa taswira za kijinamizi zinazotamausha. Wananchi wameharibu mazingira kutokana na msukumo mkali wa nguvu za kiutandawazi zinazoshinikiza biashara ya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1556

kimataifa. Bara la Afrika linafyonzwa rasilmali zake na kuachwa kuwa jangwa linalokosesha matumaini ya kuishi. Mazingira yanayorejelewa yanahusu mandhari yote yanayomzunguka binadamu. Uchafuzi wa mazingira unaunguza na kuteketeza kila eneo la maisha ya binadamu; kwa mfano, maadili, rasilmali, elimu, dini na hata utamaduni (Kevogo, 2016). Uchafuzi wa mazingira unajitokeza kutokana na matendo mabaya ya binadamu kwa binadamu mwenzake, matumizi mabaya ya elementi za mazingira kama vile vyanzo vya maji na maeneo yake, miti, hewa, wanyama na hata madini. Mazingira yanaweza kuchafuliwa iwapo maadili ya wanajamii yatadhoofika, matumizi mabaya ya kemikali kwenye maeneo ya maji kama vile mito na maziwa ambayo wakati mwengine ni makazi ya wanyama. Kwa mfano katika riwaya ya *Bina-Adamu*, kunayo sauti inayosikika ikilalamika kuhusu vitendo viovu vinavyotekelezwa huko baharini ambako kazi ya uvuvi inatekelezwa. Vitendo hivi vikiwa ni kama kumwaga mafuta kwenye maji ambayo ni makazi ya samaki wanaotengemewa kama kitenga uchumi na pia kitoweo kwa wengine. Vitendo hivi ni vya udhalimu hivi kwa samaki wauliwa ili wanaowatengemea wakawanunue kwa wengine na tena kwa bei ghali,

> *Wamemwaga mafuta hapa samaki wafe wapate sababu ya kuwaletea makopo. Huku juu wanatupa mabaki ya nyukilia.* (Wamitila, 2002, uk. 88)

Isitoshe, katika ukurasa wa 111 kuna sauti ya mhusika mwenza wa msemaji wa dondoo la hapo juu ambayo inasikika ikisema:

> *Huu ni utandu, ni mafuta yaliyomwagwa. Wanasema ilitokea kama ajali sehemu hii haina samaki wanaoishi, wamekufa wote. Kaza macho huko mbele... Je, unaona kitu chochote? Hiyo ni meli inavua samaki na kuwatia kwenye makopo kisha karibuni watakuja kuwauzia huku. Inasemwa kuwa hayo ni maji ya kimataifa* (Wamitila, 2002, uk. 111)

Kutokana na madondoo haya, ni wazi kuwa mali ya wananchi yanaharibiwa kimakusudi na wenye uwezo hivi wakiachwa kuteseka na hali zao duni na wala hakuna mtetezi. Wao wanayavumilia machungu hayo. Taswira inayojitokeza ni ya matatizo yanayowapata wananchi ambayo yanawakosesha tumaini la kuishi. Uharibifu unaoakisiwa katika madondoo haya unatokana na biashara ya kimataifa inayoendeshwa na makampuni makubwa yanayovua baharini na kuharibu mazingira kwa kisingizia cha soko huria.

Kwa upande mwingine, riwaya ya *Dunia Yao* inasawiri taathira za utandawazi kwa uharibifu wa mazingira. Mazingira yameharibika kutokana na shughuli za utandawazi na ambazo zinaporomosha utamaduni wa Kiafrika. Maadili yamezorota kwa kiasi kikubwa na ulimwengu unaelekea kuangamia iwapo hatua mwafaka hazitachukuliwa. Hali hii inaakisa katika usemi wa Ndi- anayesema kuwa:

> *Fujo. Fujo tu! Mazingira yamepopotoka. Utamaduni tusioutaka hatuwezi kuuzuia tena. Unakuja kwa mawimbi yenye nguvu. Ngono, ulevi, uchi, matusi, kelele, mavazi yakuchekesha na miili yetu inajazwa sumu. Nyama ya ng'ombe, kuku zinatisha kuliwa. Kisha ulemavu wa madawa ya kulevya na wimbi la wakimbizi linavyotishia amani ya Dunia. Vikundi vya watu wabaya vimefufuka. Tazama taathira ya vyombo vya habari na mawasiliano vinavyosambaza uhalifu. Dini… lakini nani anayejali? Kijana anyanyue bunduki kumwuua mama atoke nje kuua wapitanjia na mwisho ajimalize mwenyewe. La, si michezo ya kikatili kwenye video, DVD, na sinema si bunduki zinazoundwa na kuuzwa. Labda polisi tu hawafanyi kazi zao. Huu ndio upeo wa dunia ya leo. Dunia Yao* (Mohamed, 2006, uk. 49)

Kutokana na dondoo hili ni wazi kuwa mazingira ya kitamaduni yameathiriwa na utamaduni wa kigeni unaoenezwa na utandawazi kupitia kwa teknolojia ya habari na mawasiliano Taswira hii inaakisiwa katika Nadharia ya Usasabaadaye. Wanausasabaadaye wanaeleza kuwa, jamii inayosawiriwa katika fasihi ya Usasabaadaye

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1556

hukabiliwa na matazo yanatokana na utandawazi ambao ni mchakato wa kuunganisha uchumi, siasa, jamii na uhusiano wa tamaduni baina ya nchi. Utandawazi huwa unaifanya dunia kuwa kijiji kimoja kisicho na mipaka, kupitia kwa uondoaji wa vikwazo vya kibiashara na kuifanya dunia kuwa soko moja.

**Ubinafsi**

Waandishi wa riwaya ya kidistopia wamewasawiri wahusika wao wakiwa wabinafsi na wanaojijali wenyewe pasipo kushughulika na maisha ya wanajamii au hata aila yao wenyewe. Imekuwa vigumu sana hata katika familia ndugu kumjali ndugu, viongozi serikalini kuwajali wananchi waliowachangua au hata mzazi kumjali mwanae. Hali hii inaakisiwa katika dondoo lifuatalo linalotaoa taswira ya utengano na mwachano wa familia inayoendelea kuporomoka:

> *Wengine wote watoto wangu wapo hapahapa lakini nimewapoteza, Au, bora niseme wamenipoteza. Au tumepoteana…wapo lakini hawapo mbele ya macho yangu na mimi na mimi mbele ya wao* (Mohamed, 2006, uk. 6)

Mwandishi ameitumia familia ya Ndi- kama mfano jinsi mataifa yalivyo barani Afrika. Kulingana na historia kabla ya ujio wa wakoloni wanajamii walikuwa wakishirikiana takribani kwa kila jambo lakini baadaye walijigawa kitabaka jinsi wakoloni walivyojigawa na kuonyesha kutoshirikiana. Kwa sasa wale wasiojiweza wanaendelea na kupambana na changamoto zinazowakabili bila usaidizi wowote. Viongozi wamejitenga na raia baada ya uchanguzi na hawaajali tena. Taswira hii ya utengano wa kitabaka baina ya viongozi na wananchi inabainika katika riwaya ya Bina-Adamu kupitia kwa dondoo lifuatalo:

> *Huku ndiko wanakoishi viongozi. Hii ndio bustani yao ya Edeni, raia wakisubiri yao* (Wamitila, 2002, uk. 6)

Kutokana na dondoo hili, viongozi wamejitenga na wananchi, wanaishi maisha ya kifahari ilhali wananchi waliowachagua wanaishi katika ufukara uliokithiri. Viongozi wanayafurahia matunda ya uhuru peke yao, yaani maisha ya shamba la Edeni. Mwandishi anajaribu kuweka wazi dhamira ya viongozi kutowajibika kutokana na imani potovu kuwa wanaweza kutumia pesa walizonazo kuwahonga wapiga kura au kuwalipa vijana kuchoma kadi za uchaguzi. Taswira hii, ianjitokeza katika dondoo lifuatalo:

> *Nyie mnashikilia kusema kuwa mtaninyima kura zenu wakati wa uchaguzi? Hivi mnajua Jinsi mambo yanavyokwenda nchi hii kweli? Mtu mradi una pesa za kutosha kitakutisha nini? Nina uwezo wa kuzinunua kura zenu hizo. Chezeni tu, nitawalipa vijana kuzichoma kadi hizo za uchaguzi zinazowatia kiburi. Hivi hata lugha yenu wenyewe mmeisahau? Kitu kilivunja nguu na milima ikala* (Wamitila, 2002, uk. 141)

Maneno haya ya mwanasiasa mmoja kabla ya uchaguzi ni taswira inayomtia mwananchi hofu hivi kwamba viongozi wanaweza kutumia mbinu zozote kupata vyeo na mamlaka ya uongozi na si lazima wachanguliwe. Tamaa ya uongozi imewafanya viongozi kutotilia maanani haki za wananchi kama vile upigaji kura kuchagua kiongozi anayefaa. Umekuwa utawala wa kimabavu. Viongozi hawana maadili yanayostahili kutokana na ufisadi unaotawala. Katika riwaya ya *Dunia Yao*, wahusika ni wabinafsi na wasiowajali wenzao. Mhusika mkuu Ndi- baada ya kuporomoka katika kihali na kimali, maisha yake yanabadilika na kuchukua mkondo wa upweke na ukiwa uliokithiri. Ndi- anaamua kuitenga nafsi yake na kutoshughulika tena na jamii yake. Ikawa mwandani wake wa karibu ni kompyuta huku kajifungia chumbani mwake. Anasema:

> *Wengine wote watoto wangu wapo hapahapa, lakini nimewapoteza. Au, bora niseme wamenipoteza. Au, tumepoteana hapo lakini hawapo mbele ya macho yangu na mimi mbele ya yao* (Mohamed, 2006, uk. 6)

Kutokana na dondoo hili ni wazi kuwa Ndi- hayupo pamoja na jamii yake bali anaishi peke yake jambo ambalo halifurahii kamwe maisha

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1556

kwake hayana thamani. Taswira hii ni ya kidhamira. Mwandishi anajaribu kuonyesha matatizo yanayojitokeza kutokana na taathira za ubinafsi. Aidha, Maisha ya Mtima alikoenda huko Ughaibuni kama anavyomweleza babake kupitia barua pepe, yamejaa ubinafsi uliokithiri hivi kwamba kila mtu hubeba mzigo wake na hujitaka mwenyewe, hamtaki mwengine. Hali hii inabainika wazi katika usemi wa Mtima anaposema:

> *.....sina budi lakini kung'ang'ania. Ndivyo maisha ya huku yalivyo. Kila mtu hubeba mzigo wake. kila mtu hujitaka mwenyewe hamtaki mwingine. Ikizidi dakika moja ya kuwekwa na mtu, basi balaa.lakini utafanyaje unapokuwa huna pahala pengine pa kwenda?* (Mohamed, 2006, uk. 7)

Kutokana na usemi wa Mtima, ni wazi kuwa ubinafsi unamkosesha tumaini kuendelea kuishi huko Uingereza japo inambidi ajipe moyo na kuyavumilia machungu. Kwa kweli haya ni kinyume na matarajio ya watu wa jamii moja ambao wameunganishwa na upendo. Jamii ya Kiafrika tangu jadi ina misingi yake katika upendo, ushirikiano na umoja; haya ni maadili ya kimsingi yaliyounganisha jamii lakina yanaendele kufifia katikajamii ya kisasa. Mwandishi analenga kutahadharisha jamii ya kisasa kuhusu madhara ya ubinafsi.

**Dhuluma dhidi ya Wananchi**

Riwaya ya kidistopia inasawiri ukiukwaji wa haki za kibinadamu kama chanzo cha dhuluma kwa wananchi. Katika riwaya zote Waafrika wamesawiriwa katika kipindi cha awali wakiongozwa na mila na desturi zao wakiwa na mikakati mwafaka yakupunguza dhuluma baina yao wenyewe. Wakoloni waliimarisha dhuluma dhidi ya Waafrika kupitia kwa nguvu za ukoloni. Waafrika wakafanywa watumwa na kuuawa ovyoovyo. Ukoloni ulikita shina la ufisadi barani Afrika. Baada ya wakoloni kuondoka, Waafrika waliziendeleza dhuluma zilizokuwa zimeanza kushamiri. Hali hii inaakisiwa katika dondoo lifuatalo:

> *...kazi za ngazi za juu zilitengwa kwa wastahiki na wala hazikutegemea kuwa na elimu, akili au busara. Muhimu zaidi wewe ulikuwa nani, mtoto au mjukuu wa bwana gani na kama unaitikia 'ndiyo' kila wakati* (Mohamed, 2006, uk. 47)

Mwandishi ametumia maneno ya Ndi- kuonyesha jinsi wananchi walivyodhulumiwa huku wakinyimwa nafasi za kazi. Hali hii iliweza kudidimiza matumaini na hata maendeleo. Hata baada ya ukoloni, Waafrika waliotwaa hatamu za uongozi waliendelea kuwahini na kuwadhulumu Waafrika wenzao. Hali hii inabainika wazi katika riwaya ya *Bina-Adamu* kupitia kwa usemi wa babu anayeeleza kuwa:

> *Tulipopata uhuru tuliahidiwa kupata mashamba yaliyokuwa yamemilikiwa na wazungu. Uhuru ulikuja lakini tumeendelea kulima vikataa vyetu visivyokuwa na rutuba. Viongozi Ndio wanayoyalima hayo mashamba, uhuru wa wizi!* (Wamitila, 2002, uk. 136).

Maneno ya babu kwa msimulizi yanaonyesha kuwa wananchi wanadhulumiwa na viongozi ambao wameshindwa kuzitimiza ahadi zao. Wananchi walipata uhuru wakiwa na matumaini makubwa ya maisha yao kubadilika ila hali imekuwa kinyume. Viongozi walioshikilia uongozi baada ya wakoloni kuondoka walijilimbikizia mali ya umma hususan mashamba ambayo yangenufaisha wananchi wenzao.

**Utandawazi**

Utandawazi ni mfumo wa kimataifa unaorahisisha mawasiliano na mahusiano katika nyanja za kiuchumi, kibiashara, kisiasa, kiutamaduni na kadhalika uliojikita kwenye maendeleo ya kiteknolojia ya habari. Mfumo huu umevunja mipaka ya mataifa na kuufanya ulimwengu kama kijiji kimoja kinachoshirikiana katika nyanja tofauti za kimaendeleo (Kevogo, 2016). Utandawazi umesawiriwa kuwa na taathira hasi katika riwaya ya kidistopia. Taathira hasi za utandawazi zinashuhudiwa katika mataifa ya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1556

ulimwengu wa tatu hususan barani Afrika. Utandawazi umesababisha mfumko wa tamaduni za kigeni ambao umepotosha maadili ya Kiafrika. Hali hii inaakisa katika riwaya ya *Dunia Yao* kupitia kwa dondoo lifuatalo:

> *…lazima uukubali ukweli watoto kuanzia sasa watawaendesha wazee wao. Huu ni wakati wa wanawake kuwakimu na kuwaongoza wanaume*…. (Mohamed, 2006, uk. 25)

Maneno haya ya Yungi anayoyasema akiwa mlevi yanamchoma baba moyo. Usemi huu unaakisi taathira ya utandawazi unaochangia mmomonyoko wa maadili. Watoto ndio wanawaendesha wazazi na kufanya mambo yaliyo kinyume na misingi ya maadili ya Kiafrika.Isitoshe, kuna matumizi ya dawa za kulevya yaliyokithiri miongoni mwa vijana wanaodai kuwa kwenye dunia yao. Waafrika wameathiriwa sana na uhuru ulioletwa na utandawazi. Katika riwaya ya Bina-Adamu, taswira ya dhulima za kiuchumi zinazoendelezwa na mataifa yenye ushawishi mkubwa kiuchumi dhidi ya mataifa maskini inaonekana kupitia kwa dondoo lifuatalo:

> *Shilingi inafifia...Wameinyonga pesos…Hizi SAPS zinatusapa uhai…kijiji cha wizi hiki...Dola inatukaba shingo...Yen ni kamba ya kitanzi!* (Wamitila, 2002, uk. 137).

Isitoshe, utandawazi umehalalisha matumizi ya sarufu za mataifa yenye ushawishi mkubwa kiuchumi. Hali hii inapunja mataifa maskini kiuchumi na kuyanyima uwezo wa kushiriki kwa njia ya haki katika biashara ya kimataifa. Hili linaonekana bayana katika dondoo lifuatalo:

> *"Wanasema kuwa kuna kitu kama mizani hivi ya kupimia vitu…Mizani hiyo imeundwa kiajabu….kuna uzito fulani nasikia ni wa dollar…"* (Wamitila, 2002, uk. 142)

Madondoo haya yanatuelekeza kuhitimisha kuwa utandawazi umeidhinisha mfumo dhalimu wa soko huru hata baada ya wakoloni kuondoka, bado Waafrika wangali wanadhulumiwa kiuchumi na mkoloni aliye mbali kupitia kwa uliberali wa biashara ya kimataifa inayoendeshwa kwa dola, ambayo ndiyo sarafu inayotumika kununua na kuuza bidhaa. Pamoja na dhuluma za kiuchumi kupitia kwa dola; mfumo wa utandawazi umefungua mianya ya kufanya biashara haramu kama vile ukahaba, uporaji wa mali ya watu, ulanguzi wa dawa za kulevya na kadhalika.

**Ukoloni Mamboleo**

Baada ya wakoloni kuondoka na Waafrika kupata uhuru bado matendo na mawazo ya ukoloni yanatamalaki na kughubika bara la Afrika. Taathira za ukoloni mkongwe zingalipo na zinashuhudiwa katika kila eneo la maisha barani Afrika (Kevogo, 2016). Kuwepo kwa mikataba ya kibiashara na makampuni ya kigeni, kupokea misaada na mikopo na hata kuruhusu mashirika ya kigeni kuendesha biashara zao barani Afrika bila masharti magumu ni baadhi ya mambo yanayochangia hali za kidistopia zinazoakisi ukoloni mamboleo katika riwaya ya kimajaribio. Kwa mfano, sauti inayosikika katika dondoo lifuatalo inashadidia hali ya ukoloni mamboleo unaodhulumu Waafrika kiuchumi:

> *Shusha, shushaa…thamani ya hela shushaaa!*
>
> *Bana, Banaa….ugavi wa hela banaaa!*
>
> *Kata, kataa …matumizi ya hela kata!*
>
> *Hurisha, hurishaa…soko la hela hurishaa!*
>
> *Punguza, punguzaa…mishahara duni punguzaa!* (Wamitila, 2002, uk. 87)

Kulingana na wimbo huu wa Mefu ni wazi kuwa uhuria unaonasibishwa na utandawazi umetatiza sana maendeleo katika mataifa ya Kiafrika. Hali hii imeyafanya mataifa yanayoendelea kupororoka kiuchumi kutokana na masharti magumu yanayowekwa na wafadhili wa kigeni. Kimsingi mataifa ya Kiafrika hayana uwezo wa kufanya uamuzi wowote ila tu kuamurishwa na mataifa yaliyoendelea kuhusiana na kupanda au kushuka kwa thamani ya dola wakati wa kuendesha biashara ya kimataifa. Hii ina maana kuwa mkoloni anaendelea kumtawala Mwafrika hata baada ya wao kuondoka:

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1556

> *Nchi hii ingekuwa imepiga hatua kubwa kama ingekuwa na uongozi ufaao na kama watu wangetambua kuwa hii ni nchi yao na ya vizazi vyao wala sio jugwe la kuvuta huku na huku au zawadi la kupewa watu wanaodhani waliifanyia mengi*! (Wamitila, 2002, uk. 136)

Kulingana na dondoo hili babu anamweleza msimulizi jinsi viongozi Waafrika wamekuwa waking'ang'ania uongozi pasipo kujua kuwa hii ni nchi yao na pia vizazi vyao vinaitegemea sana siku za usoni hali ambayo imechangia sana kutojiendeleza katika sekta zilizo muhimu. Mwandishi analaumu uongozi wa bara la Afrika kwa kutowajibika na kukosa maono.

Katika riwaya ya *Bina-Adamu*, mwandishi anatumia motifu ya safari inayofungwa na Binadamu msafiri (Jagina) ambaye ni mhusika mkuu. Mwandishi amemtumia kama ishara ya taifa lililo kwenye hekaheka za kijinasua kwenye mtego wa maadui ambao ni utandawazi, ubeberu mpya na taathira za mitindo mipya ya kigeni. Safari ya Jagina inaakisi taswira za kidistopia. Ni safari ya kijinamizi inayosheheni kila aina ya hatari na maangamizi. Katika safari yake ya kinjozi inayofungwa katika ulimwengu wa kidhahania unaotawaliwa na fantasia, Jagina anakabiliwa na changamoto ya kujitambua katika ulimwengu unaobadilika kwa kasi. Jagina ni ishara ya Mwafrika aliyekosa utambulisho kutokana na taathira za utandawazi. Msafiri yuko safarini kutafuta suluhu ya matatizo ya kijiji chake kilichobaki pembezoni mwa ulimwengu. Kijiji hicho kinaashiria Mwafrika anayepambana na changamoto za dunia ya kisasa inayokabiliwa na matatizo ya kibaadaukoloni.

**Taathira Hasi za Utamaduni wa Kigeni**

Waandishi wanasawiri taathira hasi za uigaji wa tamaduni za kigeni unaofanywa kiholela na wenyeji wa bara la Afrika. Bara la Afrika limeonyeshwa katika hali ya kupoteza mwelekeo kwa kuupuza misingi bora ya maadili iliyohimiliwa katika utamaduni wa Kiafrika. Badala yake, bara la Afrika linaiga na kuthamini mitindo mipya ya maisha yenye asili ya kigeni. Waafrika wameiga utamaduni wa kigeni pasipo kufikiria kuhusu madhara ya baadaye. Mitindo ya mavazi, sherehe, matumizi ya lugha pamoja na sera za uongozi. Taswira hii inaakisiwa katika dondoo lifuatalo:

> *Jamani siku hizi kuna utalii wa aina nyingine mbaya kupindukia! Wanachotaka ni watoto wetu wa kike...wanaong'olewa shuleni kudanganya kutolewa nje…wanapewa ahadi za uongo na kuishia kuuzwa kwenye madanguro huku ughaibuni* (Wamitila, 2002, uk. 109)

Katika dondoo hili binadamu anasawiriwa kama shehena inayouzwa katika mataifa ya kigeni. Kuna ukiukwaji wa haki za kibinadamu wanawake wa Kiafrika wanapouzwa katika madanguro ya ulaya ili kuwa watumwa wa ngono. Kulingana na dondoo hili, wasichana ambao wanapaswa kujenga jamii ijayo kupitia kwa elimu ndio wanaotumika kama vyombo vya starehe na watalii. Wasichana wanawaiga watalii na kwenda kujivinjari kwenye maeneo ya starehe. Huko wanaendeleza mambo ambayo yanadhohofisha maadili kulingana na mila na desturi za waafrika. Vijana wanapatwa na magonjwa sugu pamoja na kukosa elimu. Hali hii inaendelea na kudididmiza maendeleo nchini.

> *…mara tukashtukia tunaingia katika sherehe fulani…kikwetu iliitwa fensi...'carnival' kwa lugha ya kisasa…..* (Mohamed, 2006, uk. 173-175)

Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007) *carnival* (kanivali) ni sherehe ya kitamaduni ambapo waigizaji hujivisha mafigu yafichao sura zao na wakiwa katika hali hii huigiza nyadhifa zisizokuwa zao. Mwandishi anatumia dhana hii kuonyesha jinsi Waafrika wamekubali athari za kigeni na kushawishika kwa urahisi kuupokea utamaduni wa kimagharibi. Kulingana na dondoo hili bara la Afrika linaonekana kuiga kila kitu hadi hata mitindo ya mavazi.

**Ubaguzi**

Kwa mujibu wa Kamusi ya Karne ya 21, ubaguzi ni sera au mpango wa kuhudumia watu kwa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1556

kuegemea misingi ya hadhi, kabila, elimu, rangi na kadhalika. Wakoloni walipokuwa barani Afrika waliendeleza ubaguzi wa rangi ambapo wengi wa Waafrika walitumika kama watumwa. Baada ya wakoloni kuondoka, ukafuata uongozi wa Waafrika wenyewe ambao pia ulihimili misingi na nguzo za ubaguzi ulioanzishwa na wakoloni. Mwafrika alianza kumbagua Mwafrika mwenzake. Taswira ya kijinamizi ya ubaguzi kwa misingi ya tabaka, cheo, hadhi, dini, elimu na kabila barani Afrika inabainika wazi katika riwaya ya kidistopia. Dondoo lifuatalo linabainisha hali hiyo:

> *"Tunabaguliwa tena na ndugu zetu sisi".....unaona rangi kama hii, mweusi tu kama mimi…mama nchi alipomwuliza akambaka na kumwua ndugu yetu kabisa…"* (Wamitila, 2002, uk. 91)

Kulingana na mwandishi, Waafrika wanawabagua Waafrika wenzao na kuwatendea maovu kama vile kuwabaka na hata kuwaua. Hivi kwamba hawana utu kamwe. Matendo kama haya yanawatia hofu Waafrika walio Afrika na hata wanapozuru mataifa ya ughaibuni hubaguana na kuchukiana. Taswira ya ubaguzi wa rangi inaakisiwa katika dondoo lifuatalo:

> *Nilipowaona sura zao, nilijua kuwa walikuwa watu wa nyumbani. Nadhani walinitambua pia kwani mtu wa nyumbani hafichiki, labda walikwishaniona jinsi nilivyojikunyata na kujitenga na kuwapuuza* (Mohamed, 2006, uk. 79)

Dondoo hili linasheheni maneno ya Mtima kupitia kwa barua aliyomtumia babake, ni wazi kuwa Waafrika walikuwa wanajitenga na wenzao kama vile Mtima alivyofanya akiwa safarini. Utengano huu unatokana na kujidharau na kujiona duni kutokana na kasumba ya kibaguzi iliyopandwa na wakoloni katika akili ya Mwafrika.

## HITIMISHO

Kazi hii imeangazia taswira ya distopia na maudhui ya baadaukoloni katika riwaya za kimajaribio za Kiswahili ambazo ni *Dunia Yao* (2006) na *Bina-Adamu* (2002). Tunaweza kuhitimisha kuwa, hali za kidistopia zilizosawiriwa katika riwaya hizi mbili zimesababishwa na waandishi kutamaushwa na mustakabali wa bara la Afrika ambalo limezongwa na kila aina ya uozo kuanzia umaskini, uchafuzi wa mazingira, ukoloni mamboleo, ubinafsi, dhuluma dhidi ya binadamu na utandawazi.

Katika riwaya ya *Dunia Yao* mwandishi amemtumia mhusika Ndi- kama kielelezo cha kuonyesha kuporomoka kwa bara la Afrika. Matukio yanayoshuhudiwa katika familia ya Ndi- yanalinganishwa na mataifa ya Kiafrika ambayo hupatwa na matatizo yanayotokana na wananchi wenyewe kwa kukosa kujielewa. Aidha, wananchi huisahau na kuibeza asili yao huku wakiiga mambo ya kigeni kutoka kwa mataifa yaliyoendelea katika takribani kila nyanja ya kimaendeleo. Kutoshirikiana katika ujenzi wa taifa lao na kutojikomboa kimawazo. Kulingana na mwandishi wa riwaya hii matatizo haya yanajitokeza katika uchumi, jamii, siasa, dini n.k hivi kwamba Mwafrika analo jukumu la kubadilika na wakati kwa kuzaliwa upya pamoja na jinsi ya kujiendeleza kimaisha.

Hitimisho la pili ni kuwa, makala imebainisha kuwepo kwa uhusiano wa karibu baina ya taswira za kidistopia na maudhui ya kibaadaukoloni katika riwaya mbili zilizochunguzwa. Kuzuka kwa utandawazi kumechangia kudhoofika kwa misingi ya maadili katika jamii ya Kiafrika jambo ambalo limekuza katika muktadha wa baadaukoloni. Athari za utandawazi zimeshuhudiwa sio tu upande wa kuporomoka kwa maadili, bali hata katika itikadi za kisiasa zilizokopwa kiholela. Mifumo hiyo migeni ya kisiasa inapwaya inapotumiwa katika muktadha wa Kiafrika. Bara la Kiafrika limekosa utambulisho na kujipata katika njiapanda kiitikadi, kiuchumi, kisiasa, kidini na kijamii.

Riwaya zinazochunguzwa zinawasawiri vijana 'dunia yao,' yaani ulimwengu wa kifantasia ambamo wanaonekana kutojielewa, kuasi asili yao pamoja na kuudharau utamaduni wao. Kutokana na uigaji wa utamaduni wa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1556

kimagharibi, vijana wamekuwa watumwa katika bara la Afrika. Hiki ni kinaya kwa kuwa bara la Afrika lilipata uhuru na linajitawala. Baadhi ya vijana wamesawiriwa kama waliopoteza nguzo za utambulisho wao wa Kiafrika baada ya kuangamizwa ki-utamaduni huku maadili yao yakidhoofika kwa kujihusisha na uozo hususan matumizi ya dawa za kulevya, kutowajibika na kutowaheshimu wazee jambo ambalo limechangiwa sana na utandawazi. Baadhi wameambukizwa magonjwa ya zinaa na kuishi kutawaliwa na hofu.

Waandishi wanaochunguzwa wamesawiri mustakabali wa bara la Afrika kwa hali za kidistopia. Afrika imeonyeshwa kupitia kwa jinamizi la kutisha. Kuna uozo na maangamizi yanayoporomosha bara la Afrika kwa kasi. Ukoloni uliweka nguzo ya kushamiri kwa ukoloni mamboleo. Wamitila (2002) anatumia taswira ya harufu ya beberu itapakaayo popote apitiapo kuonyesha picha halisi ya ubeberu mpya unaoenezwa kila mahali na utandawazi. Japo ubeberu mpya unaonekana kuwa mkarimu kwa kutoa misaada na kuhalalisha mikopo, lakini umeghubika hila kwa kushinikiza umaskini barani Afrika. Hii ni kwa sababu viongozi serikalini ndio kwa kiasi kikubwa wanaofurahia manufaa ya misaada na mikopo hiyo. Makampuni ya wakoloni yaliyoachwa barani bado yanazidi kunyonya rasilimali na kudidimiza maendeleo kutokana na mfumo dhalimu wa soko huria. Kibiashara duniani inaendeshwa kwa misingi ya kuwakandamiza Waafrika. Waliotwaa mamlaka na hatamu za uongozi baada ya wakoloni kuondoka wangali wanaendesha utawala wa kimabavu.

Tamaa ya uongozi, ufisadi na vitendo vingine viovu vinatekelezwa wazi; wizi wa mabavu, mauaji na hata ubakaji wa watoto wachanga umehalalishwa. Viongozi wametawaliwa na ubinafsi unaozua matabaka kadhaa. Viongozi wanaonekana wakifurahia matunda ya uhuru baada ya wakoloni kuondoka nao wananchi wanaonekana kung'ang'ania masalio ya wenye nguvu pamoja na hali zao za umaskini. Vijana wamekosa nafasi za kazi kwa sababu lazima watoe rushwa au wawe na uhusiano wa karibu na wenye vyeo serikalini.

Kimsingi ni kuwa, Wamitila na Mohamed wanapotumia mandhari ya kidistopia katika kazi zao, wanakusudia kutoa tahadhari na pia kutabiri hatari ijayo iwapo viongozi hawatawajibika kwa kutunga sera zinazostahili ili kudumisha haki za kibinadamu pamoja na utawala bora. Kwa upande mwingine, wenyeji wa bara la Afrika wanatolewa wito wa kuungana ili kuepuka hatari ya kugawanywa na kupunjwa kiuchumi na kisiasa. Waafrika wanaonywa dhidi ya kutawaliwa na ubinafsi bali washirikiane jinsi Afrika ilivyokuwa awali kabla ya ujio wa wakoloni. Utengano unaonekana kupitia kwa taswira za familia ya Ndi- iliyoparaganyika na yaliyoshuhudiwa katika kijiji cha Jagina ambapo wenyeji waliogopa kwenda kwenye kitovu na kuamua kukaa pembezoni. Taswira hizi za kimafumbo zimetumiwa na waandishi kuonyesha mustakabali wa bara la Afrika ulivyo.

## MAREJELEO

Barth, J. (1984). The literature of replenishment. In *The Friday Book: Essays and Other Fiction*. London: The Johns Hopkins University Press.

Baudrillard, J. (1988). *America*. London: Verso.

Bertoncini, E. (2016). Postmodernism in Swahili fiction and drama. In Vierke, C. & Greven, K. (Ed.), *Utopia/distopia in Swahili fiction*. Koln: Rudiger Koppe Verlag.

Diegner, L. (2016). Dunia Yao: Critical visions of the future in Swahili fiction. In Vierke, C. & Greven, K. *Utopia/distopia in Swahili fiction*. Koln: Rudiger Koppe Verlag.

Gromov, M. D. (2016). 'Local Achievement' or 'External Influence'? Intertextuality and Political Satire in the 'New' Swahili Novel in Kenya. *Dunia Yao: Utopia/Dystopia in Swahili Fiction*, 57-71.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1556

Hutcheon, L. (1988). *A poetics of postmodernism: History, theory, fiction*. New York: Routledge.

Ignatowicz, A. (2007). *Depictions dystopia in Brave New World, 1984 and Handmaid's Tale*. Unpublished thesis.

Kevogo, U.A. (2016). Taswira ya utandawazi katika riwaya mpya ya Kiswahili: Mfano wa riwaya ya Dunia Yao. *Kioo cha Lugha,* Juzuu 5, 108-126.

Longhorn Publishers (2019). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

Mohamed S.A. (2006). *Dunia Yao*. Nairobi: Oxford University Press East Africa Ltd.

Rettova, A. (2016). From memis to mize: Philosophical implications of departure from literary realism. In Vierke, C. & Greven, K. *Utopia/distopia in Swahili fiction*. Koln: Rudiger Koppe Verlag.

Traore, F.A. (2015). Postmodernism as seen through the Swahili Novel: A reading of Babu Alipofufuka and Dunia Yao by S.A. Mohamed. *Journal of African Cultural Studies*, 27:1, 20-29.

Wafula, R. na Njogu, K. (2007). *Nadharia na Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Wamitila, K. W. (2002). *Bina-Adamu*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Waugh, P. (2002). *Metafiction: Theory and practice of self conscious fiction*. London: Routledge.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.